# EPISODE 2 “LOGGING ON”

| | |
|---|---|
| **SCRIPT WRITER** | **Njoki Muhoho** |
| **EDITOR** | **Jan-Philipp Scholz** |
| **KISUAHELI:** | **Eric Ponda** |

**CHARACTERS**

| | |
|---|---|
| **ANNOUNCER** | Male Adult |
| **ZAPCOM** | A 23-year-old computer geek, by village standards. |
| **GEORGE** | 20 years old. Waits tables at his Uncle Kilu’s restaurant. |
| **MUMBI** | 22 years old, Zapcom’s cousin and social worker. Female. |
| **OMWA** | 19 years old. Secondary school leaver. Female. |
| **UNCLE KILU** | 55 years old. George’s uncle, owner of KULA TU FOODS. |
| **MANAGER** | 45 years old, the local government telecommunications company manager. Everyone calls him The Manager. |

**INTRO**

1. **MUSIC: THEME MUSIC**

***2.*** **ANNOUNCER** HUJAMBO MPENZI MSIKILIZAJI WA DEUTSCHE WELLE NA KARIBU KWA MAKALA NYINGINE YA MFULULIZO WA MCHEZO WA REDIO “LEARNING BY EAR”, ‘NOA BINGO JENGA MAISHA YAKO’.LEO TUKIZUNGUMZIA ENZI YA TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO KATIKA MCHEZO KWA JINA “KUFUNGUA MTANDAO” YAANI ***“LOGGING ON”.***

KATIKA KIPINDI KILICHOTANGULIA ZAPCOM ANABUNI WAZO LA KUANZISHA HUDUMA ZA MTANDAO WA INTANETI KATIKA MKAHAWA WA CHAKULA WA KULA TU FOODS.JE MARAFIKI WAKE WATAMUUNGA MKONO KUTIMIZA NDOTO YAKE? JE MJOMBA KILU ATALIKUBALIA KUNDI HILI LA VIJANA KUANZISHA HUDUMA HIZI KATIKA MKAHAWA WAKE? NA JE HUDUMA HIZI ZA INTANETI ZITAKUWA NA MAFUFAA GANI KWA VIJANA NA KIJIJI KIZIMA KWA JUMLA?. ENDELEA KUWA NASI HADI MWISHO WA KIPINDI UPATE KUFAHAMU MENGI TU KUHUSU AZMA YA ZAPCOM NA WENZAKE.

**SCENE 1: LOCAL PHONE SHOP.**

**3. A-SFX: <u>GENERAL NOISES OF A VILLAGE TOWN.</u>**

**4. ZAPCOM** George, kwa nini hutaki kunisikiliza ! Usinunue simu hiyo!

**5. GEORGE** **(FIRM AND ADAMANT)** Zap, nakusikiza lakini wewe huelewi.Hizi ni pesa zangu, naweza kununua simu yoyote ninayotaka!.

**6. ZAPCOM** Hebu nisikize swahiba, unahitaji simu ile, ile pale…!

**7. GEORGE** Hapana … hii ni nzuri zaidi.

**8. ZAPCOM** Hii huwezi kuunganishwa na mtandao wa Intaneti!.

**9. GEORGE** Lakini nitaweza kusikiliza redio…!

**10. ZAPCOM** Hii pia utaweza kusikiliza redio mbali na kuunganishwa na mtandao wa Intaneti.

**11. GEORGE** Nani aliweka intaneti kwenye simu hiyo!

**12. ZAPCOM** Kwani unasahau haraka vipi? Hebu tazama, tazama pale ….! unadhani mlingoti ule ni wa kazi gani? Na kwa nini unadhani unamilikiwa na kampuni ya mawasiliano ya Afritelcom?

**13. GEORGE** Ehhhee…?

**14. ZAPCOM** Wewe una masikio lakini hutaki kusikia!. Nilikwambia, kampuni za simu za mkononi hukita milingoti ya mawasiliano ya ***satellite*** ….sawa…! na kisha hebu nikukumbushe, mawasiliano ya ***satellite*** ni teknolojia ambayo, ni kama kitovu cha huduma za kupeperusha mawasiliano kupitia masafa marefu na hatimaye huduma hizo kumfikia mtu anayetumia Komputa au simu ya mkononi mahali popote alipo.

**15. GEORGE** Sawa… sawa… !Hata watu wameanza kufikiri nitatihaniwa suala hili..

**16. ZAPCOM** (**LAUGHING**) Kwani kuna ubaya? (**WITH GUSTO**). Kutoka chuo cha Zapcomology, kisha uhitimu na cheti cha shahada ya ubunifu wa miigo ya teknolojia kutoka Zapcom. (**LAUGHS**)

**17. GEORGE** Una wazimu wewe…? (**THOUGHTFUL**). Nikumbushe tena, umepanga kukutana saa ngapi na Meneja wa mawasiliano?

**18. B-SFX: RUSTLE OF CLOTHES**

**19. ZAPCOM (GASPS)** Oh hapana! Sasa angalia ulivyofanya mpaka nasahau

**20. GEORGE** Labda pia unahitaji kusomea shahada ya kumbukumbu (**EMPHASISING**)!

**21. ZAPCOM** (**SOUNDING RUSHED**) Afadhali ningeweka saa ya kengele kwenye simu yangu ya mkononi! Tuonane baadaye na kumbuka kununua simu ifaayo!

**22. C-SFX: FEET RUSHING OFF**

**23. GEORGE** (**TO HIMSELF**)… Kwani pia simu zinaweza kukukumbusha? (**SHOUTING AFTER HIM**) … Hii simu pia ina saa ya kengele yaani ***alarm***?

**24. ANNOUNCER** George anajifunza mengi na haraka kuhusu masuala haya ya teknolojia. Sasa anafahamu kuwa simu si hoja ila cha msingi ni simu atakayoweza kuwasiliana na jamaa zake na pia kuitumia kwa mawasiliano kupitia mtandao wa Intaneti. Ama kwa hakika sasa simu yake ndiyo itakayokuwa ufunguo wa ulimwengu mzima..kwani ulimwengu utakuwa mkononi mwake.

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**SCENE TWO: KULA TU FOODS**

**25. UNCLE KILU** (**ANGRY**) Umechelewa!. Kwani unakuchukua muda gani kuvuka barabara kutoka duka la upande ule wa pili? Hebu nenda jikoni haraka ukaoshe hizo sahani!

**26. GEORGE** (**ABSENT MINDED**) Ahaa

**27. E-SFX: CLATTER OF CROCKERY BEING COLLECTED FROM TABLES.**

**28. UNCLE KILU** (**ANGRY AND LOUD**) Umenisikia ? na kwa nini bado unazungusha kiuno hapa?

**29. F-SFX: FAR AWAY CRACKING OF MUSIC. MUTED. CONTINOUS**

**30. GEORGE** **(RHYTHMICALLY DANCING AND KNODDING)** Woo aha… dada… mmhu.. aha aha… yeee

**31. UNCLE KILU** **(YELLING) George!**

**32. G-SFX: MUTED MUSIC STOPS ABRUPTLY**

**33. GEORGE** Naam mjomba, umeniita?

**34. UNCLE KILU** **(VERY ANGRY).** Eti uuumeniita…? Kwani nimekuwa nikipayuka tu peke yangu kama mwenda wazimu? maskio yako umeyafunika pamba?.Na kwa nini unachezesha kiuno hapa?. Wazimu huanza hivyo! Hivyo ndivyo alivyoanza yule…yule mwenda wazimu wa hapa kijijini. … kucheza peke yake na muda si muda akaanza kukimbiakimbia uchi wa mnyama soko zima…..Au ni huyo Zapu tena..?. Anakupotosha huyo! Yeye hukuvuruga akili kila anapotoka jijini.

**35. GEORGE** (**CHEERFULLY**) Mjomba, hebu jaribu hiki chombo cha kusikizia sauti.

**36. UNCLE KILU** Nini? Mimi sina muda wa kupoteza au kucheza na biashara, wakati tunaendelea kuwapoteza wateja wanaohamia mgahawa ule mwengine…(**CONTEMPT**) ule mgahawa mpya upande wa pili wa barabara. Kama huduma zetu zitaendelea kudorora basi tutawapoteza hata wale wachache waliosalia.

**37. GEORGE** Sikiliza kidogo… hebu jaribu tu!

**38. H-SFX: MUTED MUSIC CONTINUES TO PLAY**

**39. UNCLE KILU** Ha! Kumbe uko na redio hapa…! asaaalaaaala… Kisha ni ile stesheni niipendayo… umeipata vipi stesheni hii kwenye simu yako?

**40. GEORGE** Mjomba, siku hizi unaweza kusikiliza redio kupitia simu yako ya mkononi na vile vile redio ya kawaida. Chaguo ni lako!. Aidha kutumia redio yako ya zamani au simu ya mkononi …chagua Ba- Mdogo chagua……!

**41. I-SFX: MUTED MUSIC ABRUPTLY DIES OFF**

**42. UNCLE KILU** Ha …ha..ha maajabu haya, huu ni uvumbuzi … Lakini usiniambie niitupe redio yangu ya zamani. Redio hizi za zamani bado ni nzuri sana hapa nchini. Ama kwa hakika rafiki yako Zapu ni mtu mwenye elimu. Kwanza Zapu mwenyewe yuko wapi? Ameniambia nimuekee supu ya mbuzi na sasa inaelekea kuisha! Siwezi kutengeneza nyingine kesho!

**43. GEORGE** Alienda kumuona meneja wa mawasiliano….lakini usijali mjomba, nitamjulisha. Nipe simu yangu!

**44. J-SFX: TAPPING OF A KEY BOARD**

**45. UNCLE KILU** **(LOW VOICE, CURIOUS**) Unafanya nini?

**46. GEORGE** **(DISTRACTED**). Natuma ujumbe mfupi yaani ***SMS***

**47. UNCLE KILU** Eti nini ? SOS? Kwani akikosa supu ya mbuzi ndio mwisho wa maisha?.

**48. K-SFX: TAPPING CONTINUES**

**49. GEORGE** (**CHUCKLING**) Sio ***SOS***, ni ***SMS*** – yaani ujumbe mfupi kupitia simu ya mkononi. Najaribu kumuandikia ujumbe mfupi ambao ataupata papo hapo. (TAPPING STOPS).Sawa, sasa amepata ujumbe kwamba akikawia atakosa supu aipendeyo.

**50. L-SFX: PHONE TEXT MESSAGE BEEPS**

**51. UNCLE KILU** Ni nini hiyo?

**52. GEORGE** Ni Zapcom amejibu ujumbe wangu

**53. UNCLE KILU** Ha… haraka hivyo?

**54. GEORGE** (**READING MESSAGE**). 'Nitafika katika muda wa dakika 10 hivi, ipasheni moto kwani nahisi njaa.'

**55. UNCLE KILU** **(THOUGHTFUL)** Ni nini tena chengine unachoweza kufanya kutumia simu yako? Labda, labda…kuboresha biashara yako…… nafikiria… nafikiria bado…ehhh… lakini nikiwa bado nafikiria, hebu nenda ukaoshe sahani kabla nzi hawajajazana.

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**56. ANNOUNCER** Sasa mjomba Kilu amefahamu kwamba teknolojia ya kisasa sio tu mtindo wa vijana. Pia inaweza kuboresha biashara yake. Huku George akiendelea kutafakari maajabu ya simu yake mpya mjomba Kilu anawaza jinsi ataweza kuboresha zaidi biashara yake.

**SCENE THREE: KULA TU FOODS AFTERNOON**

**57. M-SFX: DOOR OPENS. HEAVING SOUNDS.**

**58. ZAPCOM** **(BREATHLESS)** George, njoo upesi unisaidie.

**59. GEORGE** **(SURPRISED)** Zapcom, ni nini hiyo? Umepata wapi komputa?

**60. N-SFX: QUICK FEET APPROACHING. ZAPCOM HEAVING.**

**61. GEORGE** **(WHISPER)** Usiniambie umeiba kutoka kwa ofisi ya mtu. Ime…..Imechakaa hebu angalia nyaya zake zinavyoning’inia … George umeichomoa wapi hii komputa?

**62. ZAPCOM** Ni kuu kuu. Nimeinunua… Eeeeh nimeichukua kwa mkopo. Meneja amenijulisha kwa jamaa yake ambaye hivi punde ameweka mitambo mipya ya Komputa… na amekubali kuniuzia hii kuu kuu. Sasa nitaiweka katika mkahawa huu wa Kula Tu Foods..

**63. GEORGE** (**BREATHLESS**) Kwa hivyo una maana umeenda hapo tu na kui… kuichukua….. Ni nzito!

**64. ZAPCOM** Taratibu…..! Hebu, eeh tuiweke…eeeh, tuiweke pale pembeni.

**65. UNCLE KILU** Ngoja kwanza! (**WORRIED**) Nini kinachoendelea hapa? Mashini hiyo inafanya nini hapa?

**66. ZAPCOM** Hii si machine ni komputa, tunataka kuanzisha huduma za Intaneti..

**67. UNCLE KILU** **(ANGRY)**. Zapu, sasa mchezo wako unaupeleka mbali sana. Hii ni biashara yangu! Pindi unapoingia hapa lazima ufahamu kwamba umeingia katika biashara yangu. Nasikitika kwamba naendelea kuwapoteza wateja kutokana na ushindani mkali. Na sasa unakuja kuweka biashara yako hapa…unaleta wazimu wako hapa…! Hapa usoni pangu?

**68. GEORGE** Tafadhali mjomba, usikasirike... Unajua...!

**69. ZAPCOM** Sawa….hutapata mgao wa pesa zangu kutokana na biashara hii!

**70. UNCLE KILU/GEORGE** Pesa gani?

**71. ZAPCOM** Pesa gain! Zile nitakazopata kutoka kwa huduma hizi za mtandao wa Intaneti. Kwani unadhani huduma hizi ni bure?.Watu wote wanaofanya kazi hapa, wanafunzi wa sasa na hata wa zamani watalipia huduma hizi watakapokuja kusoma E-mail zao au barua-pepe, kusikiza muziki au kutazama picha. Wanafunzi wa vyuo walioko likizoni pia watagharamia huduma hizi kufanya kazi zao za utafiti.

**72. UNCLE KILU** **(THOUGHFUL AND IN FULL ATTENTION)** … Na wote hao watalipa pesa?... wote hao?

**73. ZAPCOM** Ndio. Hao wote watalipa. Kama ujuavyo, siku hizi mgahawa wako haupati wateja wengi. Mgahawa ule pale **(POINTING)** una wateja wengi kushinda huu. Tutatumia sehemu hii hapa isiyo na mwangaza wa kutosha kuweka huduma za Intaneti na ninahakika tutaongeza pato letu kuliko ilivyo sasa.

**74. GEORGE** **(EXCITED)** Mjomba, hili ni wazo zuri sana. Sasa wazee watashindana na vijana…..! (**CATCHES HIMSELF**)…Nina maana mbinu za zamani kupambana na za kisasa … (**TRAILS OFF**).

**75. UNCLE KILU** **(CAREFULLY AND CALCULATIVE**). Na wateja wenu watakuwa wakija saa ngapi?

**76. ZAPCOM** Wakati wote, biashara hii itafunguliwa kwa muda wa saa 24 kila siku kwa wiki nzima.

**77. UNCLE KILU** (**CALCULATIVE)** Na wateja hao watakula wapi?

**78. GEORGE** Hapa hapa katika mgahawa huu.

**79. UNCLE KILU** Nani atagharamia?

**80.** **ZAPCOM** **(PROUDLY)** Sisi Zapcom Café!

**81.** **UNCLE KILU** (**CALCULATIVE**) Chakula cha nani?

**82.** **GEORGE** eeeh… eeeh… wewe … chako mjomba.

**83.** **UNCLE KILU** (**DECISIVELY**) Sawa basi tumekubaliana!

**84.** **ZAPCOM** **(CONFUSED)** Kuhusu nini?

**85.** **UNCLE KILU** Hakuna chakula kitakacholetwa kutoka nje na mtalazimika kulipa kodi ya Shilingi 5,000 kila mwezi, sawa…!

**86.** **ZAPCOM** (**ALARMED**) Shilingi 5,000 za nini?

**87.** **UNCLE KILU** Kodi, Zapcom….! kwa kutumia nafasi ya mgahawa huu. Zapcom kulipa kodi ya shilingi 5,000 kwa Kula Tu Foods shilingi 5,000 kwa kutumia nafasi na vifaa vingine katika mgahawa huu?. Kweli hakuna bure siku hizi!

**88.** **GEORGE** Sawa basi tutawatumia E-mail na jumbe fupi wateja wetu wote na wale tunaotarajia, kuwafahamisha aina ya chakula kinachopatikana hapa.

**89.** **UNCLE KILU** **(EXCITED)** Mwanangu, hilo ni wazo la busara sana… ni habari njema ambazo nimewahi……

**90. ZAPCOM** Shilingi tano kila moja.

**91. UNCLE KILU** Eti nini? Pesa za nini?

92. **ZAPCOM** Ada ya ushauri wangu wa kitaalam.yaani kwa kila E-mail au ujumbe mfupi tutakaotuma kutangaza biashara yako..

**93. N-SFX: GEORGE LAUGHING LOUDLY. HAS PROBLEMS STIFFLING THE LAUGHTER. SHUFFLE AS UNCLE WALKS AWAY.**

**94. UNCLE KILU** (**MUMBLING AS HE WALKS AWAY**) Ada ya huduma za kitaalam, hehehe.. na unasahau supu ya mbuzi ninayompa kila siku?

**MUSIC: THEME MUSIC**

**OUTRO**

**95. ANNOUNCER** SASA MJOMBA KILU AMEANZA KUFAHAMU NA KUELIMIKA HARAKA KUHUSU MANUFAA YA TEKNOLOJIA YA KISASA YA MAWASILIANO KATIKA KUBORSHA BIASHARA YAKE.KWELI NI MTU ALIYEPITWA NA WAKATI HASA IKIZINGATIWA MBINU ZA ZAMANI ANAZOTUMIA KATIKA KUENDESHA

BIASHARA YAKE .HAPANA SHAKA PIA AMEFAHAMU JINSI TEKNOLOJIA YA KISASA YA MAWASILIANO INAVYOWEZA KUFUFUA NA KUBORESHA BISHARA YAKE.LAKINI JE VIJANA WATAFAULU KATIKA BISHARA HII AU NI NDOTO TU?

Ungna nasi kwa makala ijayo ufahamu yote yatakayojiri/ Pia unaweza kutembela mtandao wetu www.dw-world.de/lbe kwa maelezo zaidi kuhusu vipindi hivi vya LEARNING BY EAR Noa bongo jenga maisha yako. Ukiwa na maoni pia usisite kututumia na bila shaka itakuwa furaha yetu kusikia kutoka kwenu. Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa.